



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



TAARIFA KWA UMMA

MAPOKEZI YA FEDHA TSHS. 684,280,028 ZA MIRADI YA MAENDELEO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela **Adv.Kibamba Kiomoni Kiburwa** anautaarifu umma kuwa mnamo Tarehe **30 Juni 2023**, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, ilipokea fedha kiasi cha **Tshs. 684,280,028** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mradi wa uboreshaji wa elimu Sekondari (**SEQUIP**).

Kati ya fedha hizo, Tshs **584,280,028.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari katika kata ya Kiseke. Na fedha kiasi cha Tshs. **100,000,000.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Walimu 2 in one katika shule ya Sekondari Buzuruga

Mkurugenzi anaishukuru Serikali inayoongozwa na **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa kuipatia Ilemela fedha hizo ambazo zinaenda kuboresha mazingira ya kujifunza na kujifunzia.

Violencea S. Mbakile

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**

20 Julai, 2023

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,

Tovuti: www.ilemelamc.go.tz